TAARIFA YA KAWAIDA NA. 7284

MAMLAKA YA UDHIBITI WA USAFIRI WA ARDHINI,

TAARIFA KWA UMMA

NAULI ZA USAFIRI WA TEKSI MTANDAONA PIKIPIKI MTANDAO

Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 imeipa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini jukumu la kupanga bei au nauli za vyombo vinavyotoa huduma za usafiri ardhini. Hivyo basi, Mamlaka inautangazia umma kuhusu nauli mpya za teksi mtandao na pikipiki mtandao kama zilivyo ainishwa hapa chini-

JEDWALI LA KWANZA

NAULI ZA TEKSI MT ANDAO

(a) Teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne (4)

| NAULI | NAULI KIWANGO CHA CHINI (TZS) | NAULI KIWANGO CHA JUU (TZS) |
|---|---|---|
| Safari isiyozidi Kilomita | 3,000 | 4,000 |
| Nauli ya kuanzia safari | 500 | 1,000 |
| Nauli kwa kilomita | 800 | 1,000 |
| Nauli kwa dakika | 80 | 100 |
| Ada ya kuita usafiri(trip) | - | 3% |
| Kamisheni | 10% | 25% |
| Tozo ya LATRA | 0.5% | 1% |

(b) Teksi mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wanne (6)

| NAULI | NAULI KIWANGO CHA CHINI (TZS) | NAULI KIWANGO CHA JUU (TZS) |
|---|---|---|
| Safari isiyozidi Kilomita | 4,000 | 5,000 |
| Nauli ya kuanzia safari | 800 | 1,300 |
| Nauli kwa kilomita | 1,000 | 1,200 |
| Nauli kwa dakika | 80 | 150 |
| Ada ya kuita usafiri(trip) | - | 3.5% |
| Kamisheni | 10% | 25% |
| Tozo ya LATRA | 0.5% | 1% |

JEDWALI LA KWANZA

NAULI ZA PIKIPIKI MTANDAO

(a) Pikipiki mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi wawili (2)

| NAULI | NAULI KIWANGO CHA CHINI (TZS) | NAULI KIWANGO CHA JUU (TZS) |
|---|---|---|
| Safari isiyozidi Kilomita | 1,000 | 1,500 |
| Nauli ya kuanzia safari | 250 | 350 |
| Nauli kwa kilomita | 300 | 400 |
| Nauli kwa dakika | 50 | 70 |
| Ada ya kuita usafiri(trip) | - | 2% |
| Kamisheni | 10% | 25% |
| Tozo ya LATRA | 0.5% | 1% |

(b) Pikipiki mtandao zenye uwezo wa kubeba abiria wasiozidi watatu (3)

| NAULI | NAULI KIWANGO CHA CHINI (TZS) | NAULI KIWANGO CHA JUU (TZS) |
|---|---|---|
| Safari isiyozidi Kilomita | 2,000 | 2,500 |
| Nauli ya kuanzia safari | 350 | 500 |
| Nauli kwa kilomita | 500 | 600 |
| Nauli kwa dakika | 70 | 90 |
| Ada ya kuita usafiri(trip) | - | 2.5% |
| Kamisheni | 10% | 25% |
| Tozo ya LATRA | 0.5% | 1% |

Mamlaka inawataarifu kuwa, nauli hizi zitaanza kutumika siku kumi na nne toka tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii.

Imetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini leo tarehe 16 Mwezi 12 Mwaka 2022

JOHN STANLEY NDUNGURU
Mwenyekiti wa Bodi

TAARIFA YA KAWAIDA NA. 7285

MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINJ,

TAARIFAKWA UMMA

NAULI ZA USAF I RI WA MABASI YAENDAYO HARAKA (BRT)

Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini, Sura ya 413 imeipa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini jukumu la kupanga bei au nauli za vyombo vinavyotoa huduma za usafiri ardhini. Hivyo basi, Mamlaka inautangazia umma kuhusu nauli mpya za mabasi yaendayo haraka kama zilivyoainishwa hapa chini-

NAULI ZA USAF I RI WA MABASI YAENDAYO

| Aina ya Njia | Nauli kwa Safari (Shilingi) |
|---|---|
| Njia Kuu (Truck Route) | 750.00 |
| Njia Mlisho (Feeder route) | 500.00 |
| Njia Mlisho + Njia Kuu (Feeder + Truck Route) | 900.00 |
| Njia ya Kimara -Kibaha | 700.00 |

Vilevile, Mamlaka inawakumbusha watoa huduma za mabasi yaendayo haraka, kuzingatia masuala yafuatayo:

(a) nauli zitakazotozwa kwa ajili ya huduma ya usafiri wa mabasi ya mwendokasi zitakuwa ni zile tu zilizoainishwa katika taarifa hii;

(b) mfumo wa utoaji wa tiketi utakuwa ni wa kielekroniki (e-ticketing) na/au kwa matumizi ya kadi za malipo zitakazokubalika na mtoa huduma;

(c) kuzingatia matumizi ya kadi za malipo ikiwa ni pamoja na kutofautisha kadi zinazotumiwa na wanafnzi na kadi zinazotumiwa na watu wazima;

(d) kuwepo na utaratibu maalum wa mabasi kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya usafiri wa uhakika;

(e) mfumo wa tiketi au kadi za malipo utazingatia ukokotoaji na utunzaji wa kumbukumbu za malipo ya kodi za Serikali na tozo za mdhibiti wa huduma utaunganishwa kwenye mifumo ya utoaji wa tiketi kwa njia ya kielektroniki; na

(f) mfumo wa malipo ya nauli utaunganishwa kwenye mfumo wa leseni wa mdhibiti iii kurahisisha taratibu za udhibiti wa hudurna za mabasi husika.

Mamlaka inawataarifu kuwa, nauli hizi zitaanza kutumika siku kumi na nne toka tarehe ya kutangazwa kwa taarifa hii.

lmetolewa na Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini leo tarehe 16 Mwezi 12 Mwaka 2022

JOHN STANLEY NDUNGURU
Mwenyekiti wa Bodi